# HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI

# SHULE YA SEKONDARI KIMBIJI

S.L.P 36001
DAR ES SALAAM

MAWASILIANO

MKUU WA SHULE, **0714 387 575**

MAKAMU MKUU WA SHULE, **0714915511**

Kumb. Na…………………………

Jina la Mwanafunzi…………………………………………………………………

S.L.P……………………………………………………………………………….

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIMBIJI**

1. **Utangulizi**

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza (Form one) katika shule hii mwaka 2026 Shule ya sekondari Kimbiji ipo wilaya ya Kigamboni mkoani Dar es salaam umbali wa Km 35 kutoka katika kivuko cha kigamboni (Ferry). Usafiri wa basi kutoka Kigamboni unapatikana katika kituo cha mabasi cha Ferry Kigamboni na nauli ya mwanafunzi ni Tsh.700/=. Muhula wa kuanza masomo utaanza **13/01/ 2026** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **06/01/2026**

**Mambo ya kuzingatia**

1.1 Sare za shule

a. Sare ya shule hii ni **mashati meupe 2**, **suruali mbili (2) Bluu Bahari** kwa wavulana na **Sketi mbili (2) kwa wasichana, T-shirt moja (1) ya njano.** Maelezo ya mshono ni **Linda box kwa wasichana. Modo na vimini haviruhusiwi.**

b. Wasichana watavaa nusu kanzu kwa waislamu inayovuka kiuno.

c. Rangi ya Hijab ni nyeupe isiyo na urembo

d. Sare ya michezo kwa shule yetu ni **bukta na jezi za njano (2)** kwa wavulana na wasichana zisizokua na maandishi.

e. Kila mwanafunzi aje na Jembe lenye mpini, Kwanja na Mfagio.
**f.** Mwanafunzi aje na **RIMU** mbili (2) aina ya “**A” one,** au **Dolphin.**
g. Wanafunzi wa kike hawaruhusiwi kusuka nywele

1.2 Mwanafunzi aje na daftari, kalamu, mkebe wa hesabu na begi.

1.3 Chakula cha mwanafunzi wa kutwa, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu ni jukumu la mzazi.

1.4 Nauli ya wanafunzi wa bweni kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo, godoro na vifaa vya malazi na matibabu ni jukumu la mzazi

1.5 Mahitaji mengine ya kibinadamu kama mkanda mweusi wa ngozi, viatu vyeusi vinavyofunika miguu visigino vifupi vyenye kamba na soksi nyeupe.

**MUHIMU:**

Mzazi unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu vya masomo ya darasani (vitabu vya kiada ) vilivyo chapishwa na **Taasisi ya Elimu Tanzania (T .I . E) Tanzania Institute of Education au** vitabu vilivyo chapishwa na Oxford pia Kamusi na Oxford Dictionary (English**-**English) ni muhimu sana kwa mwanafunzi .

**MAHITAJI MUHIMU KWA WANAFUNZI WA BWENI.**

- **Wavulana:** Suruali mbili za dark blue, Track suti moja nyeusi, Tshirt mbili (2) za kijani.
- **Vifaa vingine:** Ndala nyeusi au kijani zisizozidi gharama ya Tsh. 3000/=, ndoo ndogo 1, Taulo, Bukta 2 na Tshirt 2 za njano kwa ajili ya michezo, pasi ya mkaa, sanduku la chuma, mashuka mawili ya light blue, net ya mbu nyeupe pembe nne, tochi, nguo za ndani za kutosha pamoja na godoro futi **3 inchi 6.**
- **Wasichana:** Sketi mbili darkblue linda box. Trak suti moja nyeusi, Tshirt mbili (2) za kijani, Hijabu nyeupe isiyokuwa na urembo kwa waislamu na mitandio ya zambarau ya bweni, godoro futi **3 inch 6.**
- **Vifaa vingine:** Ndala nyeusi au kijani zisizozidi gharama ya Ths. 3000/= ndoo ndogo 1, Taulo, Bukta 2 na Tshirt 2 za njano kwa ajili ya michezo, pasi ya mkaa, sanduku la chuma , mashuka mawili ya light blue, net ya mbu nyeupe pembe nne, tochi, nguo za ndani za kutosha , pads za kutosha, doti moja ya kanga kwa ajili ya waislamu, kipande 1 cha kitenge kwa wakristo.
- Vyombo vya chakula: Wanafunzi wote wa bweni wanatakiwa kuja na sahani, kijiko, bakuli dogo na kikombe.

**ZINGATIA,** vifaa tajwa hapo chini vinapatika katika maduka ya Jirani na shule hivyo unashauriwa kuja nunua kwenye maduka hayo ili kuepuka kubeba mizigo mingi KWA WANAOTOKA MBALI. (Hii ni kwa watakaohitaji huduma hii Jirani na shule)

i. T-Shirt za shule
ii. Ndoo za kuogea
iii. Counter book quire 2 na 3

**AGIZO**

1. Kila mwanafunzi ni lazima aje na ndoo yake pamoja na vyombo vya chakula.
2. Nguo za nyumbani **haziruhusiwi** shuleni, mwanafunzi atavaa sare za bweni tu kwa siku zote awapo shuleni baada ya masomo.
3. Hakuna **VISITING DAY** na kama kuna umuhimu wa mzazi kuja atapigiwa simu na mlezi wa wanafunzi.
4. Kila mwanafunzi aje na BIMA ya afya kama hana aje na Tsh. 50400/= kwa ajili ya kukatia Bima ya afya.

## SHERIA ZA BWENI

**1. Chakula**

- Utakula chakula kinachopikwa ndani ya shule tu.
- Usipeleke, usitunze, usipike au kuchemsha chakula ndani ya bweni au katika eneo la shule.
- Marufuku kukaa eneo la jiko kama sio muda wa chakula

**2. Sare za bweni**

- Utavaa sare za bweni kila siku baada ya muda wa shule na siku za mapumziko
- **Nguo nyingine haziruhusiwi. Zikibainika utanyang'anywa na hazitarudishwa.**

**3. Usafi na afya**

- Utapaswa kuwa msafi wa mwili na mavazi kila siku
- Utafanya usafi ndani na nje ya bweni kila siku.
- Utapaswa kutibiwa zahanati unapougua na kutumia dawa kwa kuzingatia maelekezo ya daktari.
- Marufuku kuwa na dawa na kuzitumia bila ya kuwa na maaelekezo ya daktari.
- Dawa za kienyeji na hirizi haviruhusiwi shuleni.

**4. Mipaka na usalama**

- Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa. Ukibainika umetoroka utafukuzwa bweni na kuwa mwanafunzi wa kutwa.

**5. Bwenini**

- Ni marufuku kumwingiza mgeni yeyote ndani ya bweni.
- Ni marufuku mwanafunzi kulala nje ya bweni.Ukibainika utafukuzwa shule
- Ni marufuku mwanafunzi kuiba vitu vya wenzake. Ukibainika umeiba utafukuzwa shule
- Ni marufuku mwanafunzi kupiga/kupigana bwenini. Ukibainika utafukuzwa shule.
- Ni marufuku mwanafunzi kwenda kwenye bweni la wanafunzi wa jinsia tofauti na yake bila ruhusa

- Ni marufuku msichana na mvulana kusimama pamoja usiku mara baada ya prepo. Ukibainika utafukuzwa shule.

2. **Sheria na kanuni muhimu za shule hii**
   Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimlimu chini ya Ofisi ya Raisi –TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.
   a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
   b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
   c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
   d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
   e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
   f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
   g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
   h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na.
   i. Kutunza mali za uma

   **2.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.**

   i. Wizi
   ii. Uasherati na ushoga
   iii. Ubakaji
   iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
   v. Kupigana au kupiga
   vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
   vii. Kudharau bendera ya Taifa
   viii. Kuwa mjamzito/Kupata mimba
   ix. Kuoa au kuolewa
   x. Kutoa mimba
   xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
   xii. Kukataa adhabu kwa makusudi
   xiii. Kuwa na simu ya mkononi

3. **Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**
    a. Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti .shuleni
    b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
    c. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

………………………

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI

## SHULE YA SEKONDARI KIMBIJI

### FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI

PICHA YA MWANAFUNZI

**A. IJAZWE NA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili la mwanafunzi ………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………
3. Taifa …………………………………………………………………
4. Uraia …………………………………………………………………
5. Dini……………………………………………………………………
6. Shule aliyo/alizo soma kabla ya kuja shule ya Sekondari Kimbiji

| Shule ya Sekondari/Msingi | Tarehe na Mwaka ulionza | Tarehe na Mwaka uliotoka |
|---|---|---|
| i. ………………………… | …………………………… | …………………………… |
| ii. ………………………… | …………………………… | ……………………………. |
| iii. ………………………… | …………………………… | …………………………… |
| iv. …………………………. | …………………………… | ……………………………. |

Saini ya mwanafunzi……………………… Tarehe……………………

**B.** MAELEZO BINAFSI YA MZAZI

PICHA YA MZAZI/MLEZI

1. Jina la Mzazi/Mlezi……………………………………………..
2. Utaifa ………………………………………………………………
3. Uraia ………………………………………………………………
4. Anuani ya DSM ……………………………………………..
   ……………………………………………………………………
5. Sehemu anayoishi……………………………………………
6. Mtaa……………………… Kata……………………………..
7. Namba ya nyumba…………………………………………
8. Simu ya nyumbani…………………… Ofisini……………………
9. Mtendaji/Mwenyekit wa mtaa
   Jina………………………………..Sahihi……………simu ………………
10. Eleza kama mtoto ana tatizo lolote kifya

…………………………………………………………………………….
……………………………………………………………………………

**C.** MAELEZO YA KIKAZI

i. Jina la mwajiri ………………………………………………………
ii. Anuani …………………………………………………………
iii. Kazi ya Mzazi/Mlezi …………………………………………………

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi……………………………………………………………………….(majina matatu)

Ambaye ni mzazi/mlezi wa…………………………………………………………

**Ninaahidi**

i. Kumpatia mwanangu mahitaji yake yote muhimu ya shule kipindi chote cha masomo yake
ii. Kusimamia na kufuatilia mahudhurio yake shuleni
iii. Kusimamia na kufuatilia maendeleo yake kitaaluma
iv. Kuhakikisha kuwa anajisomea wakati wote awapo nyumbani na kufanya mazoezi yote (Home Works) aliyopewa na walimu kufanyia nyumbani.
v. Sheria na hatua zichukuliwe dhidi yangu endapo nitashindwa kutimiza ahadi nilizoahidi hapo juu.

Jina…………………………………………………………………
Saini………………………………
Simu…………………………………
Tarehe……………………………….

KIAMBATANISHO C

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

STATION: KIMBIJI SECONDARY SCHOOL
DATE: …………………………………………………
PART A:
TO
**Medical Officer**
………………………………………………………..
………………………………………………………..
………………………………………………………..
Miss/Mr.………………………………………………………………….. Please examine the above named to his/her fitness for admission as student in the following common diseases/problems:

Put a tick (v) for a positive and cross (x) for negative in a box provided

| | |
|---|---|
| Pregnancy | |
| Asthma | |
| Worms (stool) | |
| Epilepsy | |
| TB (Tuberculosis) | |
| Sickle cell | |
| Yellow fever | |
| U.T.I | |
| Malaria | |
| hearing | |
| sight | |

Any
Other ……………………………………………………………………………………………………
…….

**PART B: MEDICAL CERTIFICAL**

To be completed by medical officer
I have examined the above named and consider that she/he is physically FIT/UNFIT admission above.
Date ……………………………………..… Signature ……………………………………………..
Station ……………………………………./ Designation ……………………………………….